GREDI YA 6 – KISWAHILI KUSOMA
Muda: Dakika 10

Soma kifungu kifuatacho kwa sauti.

TAUSI

Tausi ni ndege wa kuvutia sana. Rangi za manyoya yake huwa tofauti tofauti. Wapo tausi wenye rangi moja tu. Si ajabu kumwona tausi mweupe pepepe akitanua mabawa yake. Wapo pia tausi wenye manyoya ya rangi mseto. Tausi wengine wamejaliwa rangi nyingi mwilini. Ukiwaona utadhani kuwa unatazama upinde wa mvua. Maajabu ya maumbile!

Tausi hufikiriwa kuwa ndege mwenye maringo. Yeye hutanua mabawa yake mazuri na kuyapepeta kama njia ya kuwatumbuiza watu. Kwa kufanya hivyo, watu husema kuwa anaringa. Je, wewe unafikiri kuwa tausi ana maringo au ni hali ya maumbile tu?

Ukweli ni kuwa tausi anapendeza. Ni ndege mpole na anayetumiwa kupambia mazingira. Chakula chake ni cha ndege wa kawaida tu. Anapenda kula nafaka na wadudu. Wafugaji wengine wa tausi huwapa ndege wao chakula spesheli. Chakula hiki huwawezesha kuwa na afya. Huwafanya ndege hao kuweza kuzaana kwa wingi pia.

Mimi ninampenda na kumthamini tausi. Je, wewe?